

# Newsletter

JANUARY, 2019

ISSN 1821 - 7273 ISSUE NO. 023

## EWURA second best winner of 2017 NBAA Awards



Motto: "Fair Regulation for Positive IMPACT"

Previous issue:



## EDITORIAL BOARD

### CHAIRMAN

Mr. Nzinyangwa Mchany

### EDITOR

Mr. Titus Kaguo

### ASSISTANT EDITOR

Mr. Wilfred Mwakalosi

### REPORTERS

Ms Asiatu Msuya

Ms Tobietha Makafu

### EWURA HEAD OFFICE

4th Floor, LAPF House  
Makole Road,  
P.O. Box 2857,  
Dodoma, Tanzania  
Tel: +255 26 2329002-3;  
Fax: +255 26 2329005  
E-mail: info@ewura.go.tz

[www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)

# CONTENTS

|   |    |
|---|----|
| From the Editor .....   | 3  |
| EWURA second best winner of 2017 NBAA Awards .....                                    | 4  |
| Campaign over illegal fuel business rages on .....                                    | 5  |
| EWURA intensifies public awareness campaigns .....                                    | 6  |
| Biharamulo: An empirical example of efficiency for the country's water utilities..... | 7  |
| Quality of petroleum products strengthened .....                                      | 8  |
| Tanzanians to benefit from Natural Gas local content .....                            | 9  |
| Investment environment for electricity projects improved ....                         | 10 |
| EWURA trains Water utilities on data verification .....                               | 11 |
| Stakeholders happy on EWURA's engagement on regulatory decisions .....                | 12 |



### COVER PHOTO

EWURA's Director of Corporate Affairs, Mr. Stanley Mahembe, displays an award from the Board of Accountants and Auditors (NBAA), after the Authority emerged the second best winner of year 2017 NBAA Awards.

# From the Editor

**DEAR esteemed readers!**

I HUMBLY welcome you to join us to read our latest edition of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) Newsletter, the 23rd Edition in a series of EWURA Newsletters' publications.

This edition comes at the time when the world is celebrating the New year 2019. In the year 2018 EWURA did a wonderful job as far as regulatory issues are concerned.

As we welcome the year 2019, I am honoured to invite you to read interesting articles from various activities undertaken by EWURA for the period between September and December 2018.

EWURA regulates technically and commercially three Energy Sub-Sectors; Petroleum, Electricity and Natural Gas; and one-Water Sector; Water and Sanitation.

During the period between September and December 2018, the Authority undertook many regulatory functions some of which have been highlighted in this edition in compliance to EWURA Act, Cap 414 of the Laws of Tanzania, Section 6 (e).

The Act stipulates that the Authority shall strive to enhance the welfare of Tanzania society by enhancing public knowledge, awareness and understanding of regulated sectors including; the rights and obligations of consumers and regulated suppliers; the way in which complaints and disputes may be initiated and resolved and the duties, functions and activities of the Authority.

From the desk of the editor, I wish you a Happy, Prosperous and Blessed New Year of 2019.

**Please, enjoy reading our Newsletter!**



**Titus Kaguio**

# EWURA second best winner of the year 2017 NBAA Awards

By Asiatu Msuya

The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) has received an award from the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) for well prepared and best presented financial report for year 2017.

The award was issued to EWURA by Deputy Minister of Finance and Planning, Dr. Ashatu Kijaji, in a recently held function at APC, Bunju Dar es Salaam. EWURA's award was received by the Director of Corporate Affairs Mr. Stanley Mahembe, who was flanked by the Finance Manager, Mr. Joctan Matogo.

Speaking at the function, Dr. Kijaji said that accounts as a career, contributes in industrialization, in the sense that, it oversees use of funds, development plans and strengthens investments which foster Tanzania's vision of being the middle economy country by 2025.

After receiving the award, Mr. Mahembe, expressed

his sincere gratitude to the NBAA for recognizing the Authority, as the best institution in presenting financial statements for year 2017; and that the award is a substance to EWURA's financial management efficiency, and in complying to laws, rules and regulations.

Additionally, EWURA's Finance Manager, Mr. Joctan Matogo, emphasize that, the secret behind EWURA's success, is compliance with both national and international financial operations standards as well as conforming to the disclosure aspects in preparations and presentation of financial statements.

The Energy and Water Utility Regulatory Authority (EWURA) was among three named institutions in the Government Authorities category for best presented financial statements, following the NBAA's audit report, for year 2017.



EWURA's Corporate Affairs Director, Mr. Stanley Mahembe, receives an award for the best presented financial report for year 2017. From the Deputy Minister for Finance and Planning, Dr. Ashatu Kijaji, after the Authority became the second winner, in government Authorities category.

# Campaign over illegal fuel business rages on

By Tobietha Makafu

The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA), has continued with its campaign of curbing illegal petroleum products business.

In a more recent move, EWURA in collaboration with the Police Force, Rail Department impounded 12 fuel barrels with a total of 24,000 liters, allegedly stolen from transit product and various national projects in Ruvu Darajani and Soga areas, Coast Region.

The incident is the result of the campaign to eliminate fuel theft and smuggling initiated by the Police Force, Rail Department in collaboration with EWURA.

Assistant Commissioner of Police of the Rail Department, David Nyambugha said: "Fuel theft and illegal fuel business leads to huge loss of government revenues, as well as to individuals and oil marketing companies." EWURA's Petroleum Technical Manager, Eng. Shabani Suleiman said: "EWURA will not tolerate those who

operate oil business illegally. Doing so is illegal and one can be charged a fine not exceeding five million or sentenced to three years or both."

The Ruvu Darajani Village chairman, where the stolen barrels were found, Mr. Ally Salum Makatoka said illegal fuel business in the residential area poses threat and can be dangerous to health and the environment.

"We are very grateful to EWURA and Police Force for an initiative to expose these criminals. As the chairman of this village I will not hesitate to inform you when we find them in our area," he added.

EWURA regulates downstream petroleum sector in Tanzania mainland, to ensure it eliminates all the loopholes for illegal fuel business, and that citizens have access to quality service and products as well as to protect the health and the environment for development of the country.



Some of the barrels and jerrycans used to store stolen fuel from various projects at Soga in Kibaha.

# EWURA intensifies public awareness campaigns

By Our Reporter

The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) through its Lake Zone Offices has embarked on a strategy to enhance public education and awareness programme on the roles and functions of the Authority to its Stakeholders.

The public awareness targets top officials and public servants from the President's Office, Regional Administration and Legal Government (PO-RALG).

The Public awareness programme is intended to cover all the lake Zone regions in the Financial Year 2018/2019. EWURA Lake Zone Office covers the regions of Geita, Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga and Simiyu.

One of the key functions of the Authority is to enhance public knowledge, awareness and understanding of regulated sectors to its Stakeholders. The Authority in the cause of enhancing awareness and public education is deploying various media such as TV stations, newspapers, radio, and social media networks and website.

However, apart from using those means of communication, EWURA Lake Zone Office has decided to have face to face meetings and discussion with high level officials working with PO-RALG as part of enhancing public education and awareness to its Stakeholders.

The Communications and Public Relations Unit at EWURA Headquarters is responsible for the coordination and dissemination of public education and awareness to the public all over the country. Meanwhile the Zonal Offices are also responsible for public awareness and education in their respective Zones in consultation with the CPRU.

EWURA stakeholders includes but not limited to; Regulated Service Providers, Consumers of Regulated Services and General Public, the Central Government and its institutions and Local Government Authorities (PO-RALG), Media, Politicians and Investors.

According to EWURA Lake Zone Manager, Mr. George Mhina, a dedicated public education and awareness programme to PO-RALG officials is due to the fact that due to the nature of their activities places them close to the public especially those who are living in rural areas.

Mr. Mhina said EWURA has noted that most reported cases

on violation of licence terms and conditions, laws and rules in the Lake Zone, occurs in the rural areas which are under PO-RALG administration, therefore by creating awareness to officials working in PO-RALG will help in reducing or eliminating any future violation of the laws.

In implementation of the programme, EWURA Lake Zone Office organised and conducted special public awareness to some regions in the Lake Zone.

To start with EWURA Lake Zone Office visited Kigoma and Kagera regions, where a total of 14 District Councils were visited out of which eight were from Kigoma regions while six were from Kagera region.

Matters that were discussed with Stakeholders during the Public awareness and education programme covered but not limited to the following areas; roles and functions of the Authority, its achievements and challenges and introducing Lake Zone offices.

Stakeholders were also enlightened on how the Authority handles disputes and Complaints, the importance of using Licensed Electrical Installation Contractors, illegal buying and selling of petroleum products from unlicensed operators, how one can access petroleum products prices using mobile phones and how one can apply for license online through EWURA Licensing and Order Information System (LOIS).

During the programme, EWURA officials responded to various queries and clarified various issues that were raised.

"Public awareness education to Officials and Public Servants working with PO-RALG has been of success. There were some of the officials who had little knowledge about the Authority without knowing its role and functions and how the Authority's functions may inter relate with their functions at district. Most of them appreciated and asked for a continued cooperation between the EWURA and Local Government Authorities," explained Mr. Mhina.

Apart from conducting public awareness programme to Stakeholders, EWURA Lake Zone Office also uses Radio, TV, and newspapers operating in Lake Zone and participate in Trade Fair Exhibitions as part of its public awareness and education programmes.

# Biharamulo: An empirical example of efficiency for the country's water utilities

By Wilfred Mwakalosi

In civil service, there are some institutions that have some of the best people who work tirelessly to make their vision a reality in serving the public, despite of the challenges they may be facing. In the water sector, one of such institutions is the Biharamulo Urban Water Supply and Sanitation Authority (BUWSA).

Although it's a new organization, indications are that BUWSA is a committed institution with a wider vision towards working for its customers—who totaled 1,147 as of October 2018.

The Authority started its operations in 2004 vide a Government Gazette No. 29, 2004.

With a business license class C issued by the Energy and Water Regulatory Authority (EWURA), BUWSA is administratively under care of the Biharamulo District Council, led by a seven member board.

Production and distribution of water is facilitated by using two electrical plants from Rugango and Ruziba water sources, from where it is pumped up to reservoir tanks before distributing it by gravitational force down to consumers. BUWSA also supplies water from another source—Runyinya.

When EWURA Board visited BUWSA recently, it was told by the General Manager Mr. Siraji Basiga, that between July

and September 2018, water availability in many areas around Biharamulo urban has been satisfactory.

Contrary to the situation in the past years, customers in areas such as Uswahlilini, Majengo A, Majengo B and Sido receives water supplies for an average of 12 hours, except for customers in Rukaragata area, where water is available for 24 hours.

**However, in order to further improve its performance, BUWSA should implement its strategies to increase water production from available sources, to expand clean water network, construct water treatment facilities and to have enough reservoir tanks.**

In its report for the July to September 2018 quarter, BUWSA indicates that it has connected 42 new customers—the rate which the General Manager says it's a satisfactory average, taking into account the real situation in the area. On revenue sources, during the quarter in question, BUWSA collected a total of Tsh 55.8 million, against a target of Tsh 45.9 million—having surpassed the target for five per cent. An average monthly collection stands at Tsh 18 million.

However, in order to further improve its performance, BUWSA should implement its strategies to increase water production from available sources, to expand clean water network, construct water treatment facilities and to have enough reservoir tanks.

# Quality of petroleum products strengthened

By Asiatu Msuya

One of the prime function of the Energy and Water Regulatory Authority (EWURA), is to conduct compliance monitoring and ensure operators and petroleum facilities in the country, comply with licence terms and conditions, applicable laws, rules and standards.

As per EWURA Act Cap 414 and the Petroleum Act, 2015, Cap 392, EWURA is mandated to undertake technical, economic and safety regulatory functions in the petroleum sub-sector.

The Authority monitors wholesale and retailers to ensure that they comply with safety and quality standards and that they provide affordable service to the customers.

"EWURA is entrusted with monitoring petroleum products' quality consumed in the country to see if they conform to Tanzanian standards and specifications before allowing a supply vessel/ship to offload the products," explains Mr. Gerald Maganga, EWURA's Director of Petroleum.

On the other hand, the Authority is mandated to ensure that at all times, consumers receive quality petroleum products that conform to standards.

EWURA undertakes regular inspections to petroleum facilities and petroleum operations to ensure they comply with technical and safety requirements.

These include compliance monitoring inspections to determine if petroleum facilities and their related operations comply with applicable laws, standards, requirements of health, safety, security, quality and environment (HSSQE) and the petroleum industry best practices.

The inspection also includes sampling of petroleum products from petroleum facilities for checking marker concentration in order to find out adulteration and dumping of untaxed petroleum products into the local market.

EWURA takes punitive measures against any operators who are found to violate technical and safety requirements. These include fines, imprisonment or both.

Thorough monitoring for ensuring security and quality of petroleum product in the country is done to establish that all operators of petroleum products operate in a manner that do not pose threat to the public health, safety and the environment.

**"EWURA is entrusted with monitoring of petroleum products' quality consumed in the country to see if they conform to Tanzanian standards and specifications before allowing a supply vessel/ship to offload the products."**

# Tanzanians to benefit from Natural Gas local content

By Tobietha Makafu

The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA), is mandated to regulate the midstream and downstream natural gas and petroleum sector, which includes activities such as processing, transportation, distribution and natural gas business.

In natural gas sector, EWURA regulates the Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), TPDC, Pan African Energy Tanzania (PAET), Songas Tanzania and Maurel et Prom in downstream and mid-stream activities such as in processing plants, transportation pipes and storage facilities for natural gas conducted by TPDC as well as regulating the natural gas prices for end users.

According to EWURA's Communications and Public Relations Manager, Mr. Titus Kaguo, TPDC has to request operational license from EWURA, which is responsible for monitoring infrastructural development activities.

The Government of Tanzania has formulated the Energy Policy (2015) which stipulates that the natural gas is a resource for all Tanzanians and has to benefit the present and future generations.

"EWURA has to make sure all citizens living near the natural gas infrastructure are protected against effects resulting from natural gas activities, such as processing, distribution and business oriented", said Mr. Kaguo, adding: "many qualified citizens are with sponsored to study on natural gas."

Speaking about the Petroleum Act, Mr. Kaguo said "the Act stipulates that, citizens are encouraged and allowed to participate in natural gas activities, as well as preparing for the future employment and investment in air and land transportation, restaurants, hotels, insurance activities."

The Act also directs all companies dealing with natural gas activities, to use and purchase local commodities and materials whereby TPDC, EWURA and PURA are mandated to make sure that there is highest level of compliance.

The Natural gas sector has a very big contribution in the development of the country's economy especially on the development of industries.

**The Natural gas sector has a very big contribution in the development of the country's economy especially in this 5th government, which emphasizes on the development of industries which in big percentage depends on natural gas and electricity as a pillar for the energy.**

# Investment environment for electricity projects improved

By Asiatu Msuya

The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) has completed preparations of Model Power Purchase Agreements between Tanzania Electricity Supply Company (TANESCO) and investors.

This step will help accelerate access to electricity and promote development of small power projects (below 10 Megawatt). It will reduce negotiation time and cost, and opens the possibility of implementing rural electrification projects.

EWURA's Director of Electricity, Engineer Godfrey Chibulunje said the Authority has prepared Standardized Power Purchase Agreement and Standard Tariff Methodology, for Small Power Projects in order to attract investors for small power projects.

"EWURA has completed preparations of power prices for hydro, natural gas, coal, geothermal, solar, wind and fuel fossil energy. The initiative is meant to enhance sustainability of electricity supply for Tanzania's industrialization," said Engineer Chibulunje.

In doing so, EWURA has continued to improve investment opportunities in the electricity sub-sector aimed to hasten implementation of Tanzania's industrialization

policy.

The Authority is closely monitoring changes in the electricity sector, including those that focus to separate procedural activities and TANESCO's functions and at the same time, boost electricity production to 10,000 Megawatt by 2025.

Currently, EWURA regulates nine (9) licensed service providers which are actively carrying out power generation activities. These includes Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO); Songas Tanzania Limited; Mwenga Hydropower Limited and Tanzania Wattle Company (TANWAT).

Others are Tanzania Planting Company Limited (TPC); Tulila Hydro Electric Plant Company Ltd; Ngombeni Power Limited; Jinan Diesel Engine Company Limited; and Andoya Hydropower Company Limited.

EWURA has made significant steps in its regulatory activities through tariff setting, strengthening license application system, and compliance monitoring to ensure quality and reliability of services and supplies in the electricity sub-sector.

# EWURA trains Water utilities on data verification

By Asiatu Msuya

The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) has conducted training to the management of Water and Sanitation Authorities (WSSA) in the country on how best they can verify their reports, one of the pre-requisites for EWURA in the preparations of Annual Performance Report of WSSAS.

Opening the consultation meeting, EWURA's Director of Water and Sanitation, Eng. Exaud Fatael, said the meeting objective was to ensure that stakeholders in the water sector are aware of how the Authority prepares water sector performance reports.

"Our ranking criterion is transparent and aims to ensure that the WSSAs strengthen revenue collection, service delivery and are consistent to quality standards," said Eng. Fatael.

Eng. Fatael also urged the WSSAs to prepare client service charter and share the same with their customers to ensure that they understand their rights and obligations in obtaining their services.

"This year's (2019) performance ranking of WSSAs will also gauge the existence of a client service charter," insisted Eng. Fatael.

More than 100 stakeholders from the Ministry of Water, Presidents' Office-Regional Administration and Local Government (TAMISEMI) and executives from District, Regional, Township WSSAs and national water projects attended the consultative meeting which was held in Dar es Salaam.

11



Participants from Regional Water Utilities and National projects, in a group photo, after attending a consultative meeting conducted by EWURA in Dar es Salaam recently.

# Stakeholders happy on EWURA's engagement on regulatory decisions

By Tobietha Makafu

Stakeholders are happy with the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA), decision to fully engage its stakeholders in regulatory decision making process on issues that direct impact their lives.

Stakeholder's engagement is employed through public inquiry in making important decisions, especially in setting tariffs for water, electricity and liquefied petroleum gas.

Public inquiry is a process of making a thorough investigation before making decisions. Through public inquiry, EWURA seeks opinion from key stakeholders of regulated services and this is provided in the EWURA Act.

In such process, recently EWURA conducted public inquiry meetings to adjust water tariff for Water and Sanitation Authorities in Ngara, Mpwapwa, Shinyanga, Wanging'ombe, and Geita. Others are Bunda, Karagwe, Turiani, Kigoma, Urambo and Makonde.

Speaking on behalf of EWURA's Director General, during the water public inquiry held at Wanging'ombe, Njombe region, EWURA's Southern Highland Manager, Eng. Karim Ally, said: "The system of public inquiry is one among the Government strategies of fulfilling good governance and transparency."

**In such process, of recently EWURA has conducted public inquiry meetings to adjust water tariff for Water and Sanitation Authorities in Ngara, Mpwapwa, Shinyanga, Wanging'ombe, and Geita. Others are Bunda, Karagwe, Turiani, Kigoma, Urambo and Makonde.**

Commenting after the public inquiry session, Ms. Fatuma Mwakifulefule, a Wanging'ombe resident said: "We thank EWURA for conducting this meeting, it will be good if those benefits mentioned by the Water Authority be real that they will improve the water quality and services."

After collecting stakeholder's opinions, EWURA conducts a thorough analysis in order to make sure the decision made will not favor any part.

According to EWURA's act, If one is not satisfied with EWURA's descisions, one has the right to appeal to the Fair Competition Tribunal (FCT).

# Newsletter

JANUARI, 2019

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 023

## EWURA yang'ara tuzo za NBAA 2017



Jarida lililopita:



## BODI YA WAHARIRI

### MWENYEKITI

Bw. Nzinyangwa Mchany

### MHARIRI

Bw. Titus Kaguo

### MHARIRI MSAIDIZI

Bw. Wilfred Mwakalosi

### WAANDISHI

Bi. Asiatu Msuya

Bi. Tobietha Makafu

### MAKAO MAKUU YA EWURA

Ghorofa ya 4,  
Jengo la LAPF Pension Fund,  
Barabara ya Makole,  
S.L.P. 2857,  
Dodoma, Tanzania  
Simu: +255 26 2329002-3,  
Nukushi: +255 26 2329005,  
Barua pepe: info@ewura.go.tz

[www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)

# YALIYOMO

|   |    |
|---|----|
| Kutoka kwa Mhariri.....   | 3  |
| EWURA yang'ara tuzo za NBAA 2017 .....                                  | 4  |
| Mapambano dhidi ya soko holela la mafuta yaendelea .....                | 5  |
| EWURA yaongeza nguvu utoaji wa elimu kwa umma .....                     | 6  |
| Biharamulo: Kielelezo bora cha ufanisi kwa Mamlaka za maji nchini ..... | 7  |
| Ubora wa mafuta ya petroli unavyodhibitiwa .....                        | 8  |
| EWURA inavyodhibiti gesi asilia.....                                    | 9  |
| Mazingira uwekezaji miradi ya umeme yaboreshwa .....                    | 10 |
| EWURA yazipiga msasa Mamlaka za Maji kuhakiki taarifa.....              | 11 |
| Wadau wafurahishwa ushirikishwaji kwenye uamuzi .....                   | 12 |



PICHA YA MBELE

Mkurugenzi wa Fedha, Raslimaliwatu na Utawala wa EWURA, Bw. Stanley Mahembe, akionesha tuzo ambayo Mamlaka ilipewa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) baada ya kuibuka mshindi wa pili kwa mwaka 2017.

# Kutoka kwa Mhariri

**Mpenzi Msomaji wetu!**

Kwa unyenyekevu, ninakukaribisha kusoma jarida letu la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) toleo la 23, katika mfululizo wa Majarida ya EWURA.

Jarida hili linakuja wakati ambapo ulimwengu unasherehekea mwaka mpya wa 2019. Mwaka 2018 ulikuwa wa mafanikio makubwa kwa EWURA kutokana na kazi nzuri iliyofanywa kwenye masuala ya udhibiti.

Wakati tunaingia kwa mafanikio mwaka mpya wa 2019, nakukaribisha kusoma taarifa za kuvutia kuhusu shughuli za EWURA katika kipindi cha mwezi Septemba hadi Desemba 2018.


EWURA inadhibiti kiufundi na kibashara sekta ndogo tatu za Nishati ambazo ni Petrol; Umeme na Gesi Asilia na Sekta moja ya Maji na Usafi wa Mazingira.

Katika kipindi cha Septemba hadi Desemba 2018, EWURA ilifanya shughuli mbalimbali za kiudhibiti ambazo baadhi yake, zimechapishwa katika toleo hili, kwa mujibu wa Sheria ya EWURA Sura na 414 ya Sheria za Tanzania, kipengele cha 6(e).

Kipengele hicho kinaelekeza wajibu wa Mamlaka kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa pamoja na haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; Njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za mamlaka kwa ujumla.

Ninawatachia kila la heri katika mwaka 2019; uwe wa mafanikio na baraka tele.

**Heri ya Mwaka Mpya 2019!  
Furahia usomaji wa Jarida letu**



**Titus Kaguo**

# EWURA yang'ara tuzo za NBAA 2017

By Asiatu Msuya

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeshinda tuzo na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), kwa kuwa mshindi wa pili katika uandaaji na uwasilishaji bora zaidi wa taarifa ya fedha, kwa mwaka 2017.

Tuzo hiyo ilitolewa hivi karibuni na Naibu Waziri wa Fedha, Daktari Ashatu Kijiji, katika hafla iliyofanyika katika Kituo cha Uhasibu na Ukaguzi cha NBAA, Bunju, Dar es Sar es Salaam na kupokelewa na Mkurugenzi wa Fedha, Rasilimali Watu na Utawala wa EWURA, Bw. Stanley Mahembe.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dkt. Kijiji, alisema taaluma ya uhasibu ina mchango mkubwa katika uchumi wa viwanda, kwa kuwa inahusika moja kwa moja na udhibiti wa matumizi ya fedha, usimamizi wa mipango, pamoja na kuimarisha mazingira ya uwekezaji kuelekea katika uchumi wa kati ifikapo 2025.

Baada ya kupokea tuzo hiyo, Bw. Mahembe alitumia fursa hiyo kuishukuru NBAA kwa kuipatia EWURA tuzo, na kueleza kuwa itakuwa chachu ya kuifanya Mamlaka kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha na uandaaji wa hesabu kwa mujibu wa sheria, taratibu na miongozo mbalimbali.

Naye Meneja wa Fedha wa EWURA, Bw. Joctan Matogo, ambaye alihudhuria hafla hiyo, alisema ushindi wa EWURA umetokana na kufuata miongozo ya kitaifa na kimataifa katika uandaaji wa hesabu pamoja na kutoa maelezo ya ziada yanayofafanua vizuri zaidi na kwa undani hesabu na utendaji kazi wa Mamlaka.

EWURA ni mongoni mwa taasisi tatu bora kuwa na hati safi ya taarifa za fedha kwa upande wa Mamlaka nchini, kwa mujibu wa ukaguzi uliofanywa na NBAA kwa mwaka 2017.



Mkurugenzi wa Masuala ya Fedha na Utawala wa EWURA, Bw. Stanley Mahembe akipokea tuzo kutoka kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijiji, baada ya EWURA kuibuka mshindi wa pili, ngazi ya Mamlaka, katika uwasilishaji mzuri wa taarifa za fedha kwa mwaka 2017.

# Mapambano dhidi ya soko holela la mafuta yaendelea

By Tobietha Makafu

**M**amlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeendelea na mapambano ya udhibiti wa uuzwaji holela wa bidhaa za mafuta aina ya petroli, kwa wanaofanya biashara hiyo kinyume cha sheria.

Hivi karibuni, EWURA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kitengo cha Reli, ilikamata mapipa 12 yenye ujazo wa jumla ya lita 24,000 za mafuta aina ya dizeli yanayodaiwa kuibwa kutoka katika magari ya kusafirisha mafuta na miradi mbalimbali eneo la Ruvu darajani na Soga mkoani Pwani.

Kukamatwa kwa mapipa hayo kumetokana na kampanya ya kutockomeza wizi wa mafuta ilioanzishwa na Jeshi la Polisi kitengo cha Reli kwa kushirikiana na EWURA.

Kamishna Msaidizi wa Polisi kitengo cha Reli nchini, David Nyambugha alisema Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamatwa baadhi ya watu wanaojihusisha na biashara hiyo, katika operesheni hii ya kudhibiti wizi wa mafuta.

“Wizi huu unatia hasara Serikali, watu binafsi na wafanya biashara wenye vituo rasmi, kwa sababu mafuta hayo huuzwa kwa bei ya chini tofauti na bei halali iliyopangwa na EWURA,” alisema.

Kwa upande wa EWURA, Meneja wa Ufundini Kitengo cha Mafuta EWURA, Mhandisi Shabani Suleiman alisema EWURA haitavumilia wanaofanya biashara ya mafuta katika vituo bubu na maeneo mengine yasiyoruhusiwa. “Kufanya hivyo ni kunyume cha sheria na adhabu yake ni kulipa faini kiasi kisichozidi milioni tano au kifungo cha miaka mitatu jela,” alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ruvu, yalipokamatwa mapipa hayo ya mafuta, Bw. Ali Salum Makatoka alisema: “Hii ni mara yangu ya kwanza kuona kituo bubu kikiuza mafuta katika eneo langu, tena katika makazi ya watu, jambo ambalo linaweza kuwa hatari kwa afya na mazingira.”

Alongeza: “Tunashukuru sana EWURA na Jeshi la polisi kwa kuwafichua wahalifu kama hawa ambao wanarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. Mimi kama Mwenyekiti wa kijiji hiki sitasita kutaarifi watusiwa endapo tutashuhudia uhalifu mwingine kama huu.”

EWURA imepania kuendelea kudhibiti mkondo wa chini wa sekta ya petroli kwa kuhakikisha inaondoa mianya yote ya wizi, ili watumiaji wa bidhaa hizo wapate huduma iliyobora, kulinda afya pamoja na mazingira kwa maendeleo ya Watanzania.



Baadhi ya vyombo viliyyotumika kuhifadhi mafuta yaliyoibwa katika miradi mbalimbali eneo la Soga, mkoani Pwani.

# EWURA yaongeza nguvu utoaji wa elimu kwa umma

## Na Mwandishi Wetu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepania kutoa elimu kuhusu utekelezaji wa majukumu yake na dhana nzima ya udhibiti. Pamoja na kutoa elimu kwa umma kwa ujumla, msukumo wa elimu hii pia utawalenga viongozi na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Kwa kuanzia, programu hii itaanzia katika Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Ofisi ya EWURA ya Kanda ya Ziwa ina hudumia mikoa saba ambayo ni Mwanza, Shinyanga, Mara, Kagera, Geita, Simiyu na Kigoma.

Moja ya majukumu ya EWURA ni kutoa elimu kwa wadau wake kuhusu kazi na majukumu ya Mamlaka kwa sekta inazozidhibiti. Elimu hutolewa kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kama luninga, magazeti, redio na mitandao. Hata hivyo, pamoja na kutumia njia hizo zote za mawasiliano, Ofisi ya EWURA Kanda ya Ziwa itazitembelea na kutoa elimu ya ana kwa ana ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Kanda ya Ziwa.

Elimu kwa Umma kwa sehemu kubwa imekuwa ikitekelezwa vizuri kwa ngazi ya kitaifa kupitia kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Umma makao makuu. Hata hivyo, Ofisi za Kanda zinawajibu pia wa kutoa elimu kwa wadau wake kwa ushirikiano na kitengo cha Mawasiliano makao makuu.

Ifahamike kuwa wadau wa EWURA ni pamoja na watoa huduma zinazodhibitiwa na EWURA, watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Wizara, Idara za Serikali, Mashirika ya Umma, Serikali za Mitaa, Vyama vya Kiraia, Vyombo vya habari, Wabia wa Maendeleo, Wawekezaji, Wanasiasa na wananchi kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Meneja wa EWURA kanda ya Ziwa Bw. George Mhina, uamuzi wa kuzitembelea Ofisi za TAMISEMI, kwa ajili ya kutoa elimu unatokana na ukweli kuwa viongozi wa TAMISEMI na watendaji wao wapo karibu zaidi na wananchi hasa wale waishio vijijini, hivyo endapo viongozi hao wataelewa kazi na majukumu ya EWURA, ni dhahiri kuwa elimu hiyo itawafikia wananchi walio wengi kwa haraka.

Bw. Mhina amesema EWURA imebaini ukiukwaji wa sheria,

kanuni na taratibu ambao mara nyingi hutokea maeneo ya vijijini ambayo yapo chini ya TAMISEMI, hivyo kutoa elimu kwao kunaweza kusaidia kuzuia ukiukwaji huo unaofanywa na watoa huduma wa sekta za nishati na maji.

Katika kutekeleza azma hiyo, tayari EWURA Kanda ya Ziwa imefanya ziara maalum ya kutoa elimu kwa umma na kuzitambulisha Ofisi za Kanda ya Ziwa. Kwa kuanzia, EWURA Kanda ya Ziwa imefanya ziara katika mikoa ya Kigoma na Kagera, kuanzia tarehe tarhere 29 Oktoba hadi 10 Novemba 2018.

Katika ziara hiyo, jumla ya halmashauri za Wilaya 14 zilitembelewa, kati ya hizo, nane ni za Mkoa wa Kigoma na sita za Mkoa wa Kagera. Aidha mkoani Kigoma, ziara ya maafisa wa EWURA ilijumuisha pia kutembelea ofisi ya Kamanda wa Polisi wa mkoa na kufanya mazungumzo na Maafisa wa Jeshi la Polisi mkoani humo.

Elimu iliyotolewa katika ziara hiyo ni pamoja na kuitambulisha EWURA na majukumu yake, mafanikio, changamoto na kuzitambulisha ofisi za Kanda. Aidha wadau pia walielimishwa jinsi EWURA inavyoshughulikia malalamiko kwenye sekta za nishati na maji, umuhimu wa kutumia wakandarasi wa umeme wenye leseni za EWURA, athari za kutumia mafuta yanayouzwa kiholela, jinsi ya kuzipata bei kikomo zinazotangazwa na EWURA kwa kutumia simu za mikononi na jinsi ya kuomba leseni kwa kutumia mtandao.

Katika ziara hiyo EWURA ilijibu hoja mbalimbali na kutoa ufanuzi katika masuala ya nishati na maji kwa watendaji hao.

“Kwa kweli elimu kwa viongozi na watendaji wa TAMISEMI ilikuwa ya mafanikio makubwa. Wapo watendaji ambao walikuwa wanaisikia EWURA, bila kujua kwa undani kazi zetu, hivyo wengi walishukuru kwa elimu tuliyowapa kwani waliweza kuifahamu EWURA kwa undani,” alieleza Bw. Mhina.

Mbalii ya ziara kama hizo, EWURA kanda ya Ziwa imekuwa ikitoa elimu kwa umma kwa kutumia redio na luninga zinazosikika kwenye kanda hiyo, pamoja na kushiriki kwenye maonesho mbalimbali.

# Biharamulo: Kielelezo bora cha ufanisi kwa Mamlaka za maji nchini

Na Wilfred Mwakalosi

**K**atika kuwatumikia wananchi, zipo baadhi ya taasisi ambazo zina watumishi wenyewe ari na maono ya juu katika kuwashudumia wananchi, licha ya changamoto lukuki zinazoweza kuwakabili. Katika sekta ya maji, moja ya taasisi hizo ni Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Biharamulo Mjini, au BUWSA.

Ingawa ni taasisi changa, BUWSA imeonesha kuwa na mtazamo wenyewe kutia moyo katika kuwashudumia wateja wake, ambao hadi kufikia mwezi Oktoba 2018, idadi yao ilikuwa 1,147. Mamlaka hii ilianzishwa Mwaka 2004 kwa tangazo la serikali namba 29, 2004.

Mamlaka hii yenye leseni Daraja C iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kwa sasa inalelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, ikiongozwa na Bodi yenye wajumbe saba.

Uzalishaji na utoaji huduma ya maji Biharamulo hufanywa kwa kutumia mitambo miwili inayoendeshwa kwa umeme, kutoka kwenye chanzo cha maji cha Rugango na Ruziba, ambako huyapeleka maji kwenye matanki, kabla ya kusambazwa kwa mserereko hadi kwa wateja. BUWSA inasambaza maji pia kutoka chanzo kingine cha Runyanya.

Bodi ya EWURA ilipotembelea Mamlaka hiyo hivi karibuni, ilielezwa na Meneja Mkuu wa BUWSA,

Ndugu Siraji Basiga, kuwa katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2018, hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ya mjini Biharamulo ilikuwa nzuri.

Ikilinganishwa na miaka ya nyuma, Meneja huyo anasema kwa sasa wateja wa maeneo ya Uswahilini, Majengo A, Majengo B na Sido wanapata maji kwa wastani wa saa 12—isipokuwa wateja wa eneo la Rukaragata, ambako hupata maji wakati wakati wote.

Katika taarifa yake ya robo mwaka kuanzia Julai hadi Septemba 2018, BUWSA imefanikiwa kuunganisha wateja 42—idadi ambayo Meneja anasema si haba ukizingatia hali halisi ya Biharamulo.

Kwa upande wa mapato, kwa kipindi cha robo mwaka taasisi ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 55.8 milioni, ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi 45.9 milioni—ikiwa imevuka lengo kwa asilimia tano. Wastani wa makusanyo ni shilingi milioni 18 kwa mwezi.

Hata hivyo, ili kuimarisha utendaji wake, BUWSA inatakiwa kutekeleza mikakati ya kuongeza uzalishaji wa maji kutoka katika vyanzo vilivyopo, kupanua mtandao wa majisafi, kuwa na mitambo ya kutibu maji na matenki ya kutosha ya kuhifadhi maji kabla ya kuyasambaza.

**Mamlaka hii  
yenye leseni Daraja C  
iliyotolewa na Mamlaka  
ya Udhibiti wa Huduma za  
Nishati na Maji (EWURA),  
kwa sasa inalelewa na  
Halmashauri ya Wilaya  
ya Biharamulo, ikiongozwa  
na Bodi yenye  
wajumbe saba.**

# Ubora wa mafuta ya petroli unavyodhibitiwa

By Asiatu Msuya

**M**oya ya majukumu ya msingi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ni kuhakikisha wafanyabiashara ya mafuta wanifuata sheria, kanuni na kukidhi viwango nya ubora katika utoaji huduma za mafuta nchini.

Sheria ya EWURA na Sheria ya Petroli zinaipa EWURA mamlaka ya kudhibiti masuala ya kiufundi, kiuchumi na kiusalama katika sekta ya petroli.

"EWURA husimamia wauzaji wa jumla na rejereja wa mafuta ili kuhakikisha wanatoa huduma yenye ubora na viwango vinavyostahili na kwa gharama ambayo watumia huduma hiyo wanaimudu," anaeleza Mkurugenzi wa Petroli wa EWURA, Mr. Gerald Maganga.

EWURA pia ina jukumu la kuhakikisha kuwa mafuta yanayotumika nchini yanakidhi viwango nya ubora kama vilivyoanishwa na Shirika la Viwango (TBS) kabla mafuta yalipokelewa kutoka nje ya nchi hayajaingia katika matumizi.

Wafanyabishara ya mafuta nao wana wajibu wa kuhakikisha kuwa bidhaa zao wakati wote zinazingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

EWURA hufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo nya mafuta, maghala ya kuhifadhia mafuta na katika magari ya kusafirishia mafuta ili kujiridhisha endapo uendeshaji wa biashara ya mafuta,

**EWURA hufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo nya mafuta, maghala ya kuhifadhia mafuta na katika magari ya kusafirishia mafuta ili kujiridhisha endapo uendeshaji wa biashara ya mafuta, unazingatia masuala muhimu ya kiufundi na kiusalama.**

magari ya kusafirishia mafuta ili kujiridhisha endapo uendeshaji wa biashara ya mafuta, unazingatia masuala muhimu ya kiufundi na kiusalama.

Ukaguzi huo pia huhusisha kujiridhisha kuwa taratibu za kisheria na kanuni za uendeshaji biashara zinafuatwa kikamilifu.

Mamlaka huchukua sampuli za mafuta ili kujiridhisha endapo bidhaa za mafuta zilizo sokoni zinakidhi viwango nya ubora na ni salama kwa matumizi. Hii inafanyika kwa kupima wingi wa vinasaba katika mafuta ya soko la ndani ili kujiridhisha kuwa hakuna uchakachuaji, udanganyifu au ukwepaji wa kodi za Serikali.

Unapobainika ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu za kiufundi na kiusalama katika uendeshaji wa biashara ya mafuta, EWURA huchukua hatua kali dhidi ya mhusika. Hatua hizo zinawenza kuwa faini, kifungo au vyote.

EWURA hufanya ufuutiliaji kwa umakini wa hali ya juu wa uendeshaji wa biashara ya mafuta nchini kwa lengo la kuhakikisha huduma inayotolewa inamlinda mtumia huduma dhidi ya madhara ya kiafya, kiusalama na kimazingira.

# EWURA inavyodhibiti gesi asilia

By Tobietha Makafu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatambuliwa kuwa mdhibiti huru katika mkondo wa kati na chini (kuchakata, kusafirisha, kusambaza na biashara) ya gesi asilia na mafuta.

Katika sekta ya gesi asilia, EWURA inazidhibiti taasisi zinazohusika na kuchakata, kusafirisha, kusambaza na kufanya biashara ya gesi asilia.

Taasisi hizi ni Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Pan African Energy Tanzania (PAET), Songas Tanzania na Maurel et Prom.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mawasiliano na Uhushiano EWURA, Bw. Titus Kaguo kampuni hizi huomba na kupatiwa leseni mbalimbali na EWURA, ambayo hufuatilia uendelezaji wa miundombinu (mitambo ya kuchakata, mabomba na maghala ya kuhifadhi) gesi asilia, utendaji na kuitisha maombi ya tozo na bei za gesi asilia kwa wateja wa mwisho.

Ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na shughuli za gesi asilia kwa wananchi wa maeneo husika na kuwaacha masikini, Serikali ilipitisha sera ya Nishati (2015) kuwa gesi ya Tanzania ni mali ya Watanzania wote, na itatumika kwa manufaa ya Watanzania wote.

"Hivyo EWURA imejipanga vyema kulinda maslahi ya Watanzania, ili athari zinazoweza kujitokeza kutokana

na shughuli za gesi asilia, ikiwamo uchakataji na usambazaji zisisababishe madhara kwa wananchi wanaozunguka," alisema Bw. Kaguo.

Katika kufanikisha hilo, elimu ya vyuo vikuu imekuwa ikitolewa bure kwa wazawa wenye sifa ili kuongeza wataalam kwenye kada ya gesi asilia, na taarifa za utekelezaji zinasambazwa kila mara mionganini mwa wadau.

Akizungumzia Sheria ya Mafuta (2015), Bw. Kaguo alisema inataka wazawa washirikishwe katika masuala yote ya gesi asilia na watayarishwe vizuri ili waajiriwe katika shughuli za gesi asilia, pamoja na uwekezaji katika shughuli saidizi kama huduma za chakula, hoteli, bima na nyingezeo.

"Sheria pia inatoa masharti kwa kampuni zote za kigeni zinazojihusisha na shughuli za gesi asilia kununua bidhaa za hapa nchini ambapo TPDC, EWURA na PURA zimepewa jukumu la kufuatilia," aliongeza.

Sekta ya gesi asilia imekuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa taifa hasa katika kipindi hiki cha ujenzi wa uchumi wa viwanda, ambapo kwa kiasi kikubwa huhitaji nishati za gesi na umeme kama mhimili muhimu ya sekta hiyo.

# Mazingira uwekezaji miradi ya umeme yaboreshwaa

By Asiatu Msuya

Li kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kwenye uwekezaji wa miradi midogo ya kuzalisha umeme (chini ya Megawati 10), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeandaa mikataba elekezi ya kuuziana umeme (Model Power Purchase Agreements) kati ya TANESCO na wawekezaji.

Mikataba hii, pamoja na masuala mengine hupunguza muda wa majadiliano kati yao na inawezesha uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Mkurugenzi wa masuala ya Umeme wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje amesema EWURA imeandaa mikataba maalumu ya kuuziana umeme (Standardised Power Purchase Agreement) na kanuni za kupanga bei ya umeme (Standardised Tariff Methodology) kwa lengo la kuvutia wawekezaji katika miradi midogo ya Umeme.

“EWURA imetayarisha bei elekezi za ufuaji umeme utokanao na maji, gesi asilia, makaa ya mawe, jotoardhi, umeme wa jua, upepo na mafuta ili kuiwezesha Tanzania kuwa na umeme wa uhakika kwa matumizi ya viwanda,” anasilitiza Mhandisi Chibulunje.

Hatua ya hizi ni sehemu tu ya jitihada kubwa

zinazofanywa na EWURA katika kuimarisha mazingira ya kuvutia uwekezaji katika miradi ya umeme ili kushajihisha utekelezaji wa sera ya viwanda.

Mamlaka imeendelea kuratibu mabadiliko katika sekta ndogo ya umeme (ESI) ambayo yanalenga kuongeza uwezo wa uzalishaji kufikia Megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025.

Kwa sasa EWURA inadhibiti jumla ya watoa huduma 9 ambaa ni Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO); Songas Tanzania Limited; Mwenga Hydropower Limited na Tanzania Wattle Company (TANWAT).

Wengine ni Tanzania Planting Company Limited (TPC); Tulila Hydro Electric Plant Company Ltd; Ngombeni Power Limited; Jinan Diesel Engine Company Limited na Andoya Hydropower Company Limited.

Katika kutekeleza majukumu yake ya kiudhibiti, EWURA imeboresha huduma za utoaji leseni za umeme kwa kuimarisha mfumo wa uombaji leseni kwa njia ya mtandao yaani LOIS, upangaji wa bei pamoja na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa.

**“EWURA imetayarisha  
bei elekezi za ufuaji umeme  
utokanao na maji, gesi asilia,  
makaa ya mawe, jotoardhi,  
umeme wa jua, upepo  
na mafuta ili kuiwezesha  
Tanzania kuwa na umeme  
wa uhakika kwa  
matumizi ya viwanda.”**

# EWURA yazipiga msasa Mamlaka za maji kuhakiki taarifa

By Asiatu Msuya

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekutana na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuhakiki taarifa zao za utekelezaji wa majukumu ili kuiwezesha EWURA kuandaa taarifa ya utendaji kazi wa Mamlaka kwa mwaka 2018.

Akifungua kikao hicho, Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa EWURA, Mhandisi Exaud Fatael, alisema kikao hicho kiliandaliwa ili kuhakikisha wadau wote wa sekta ya maji wanapata uelewa wa namna EWURA inavyoandaa taarifa za kiutendaji kazi na ushiriki wao pamoja na vigezo vinavyotumika kupima utendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini.

"Mpango wetu wa kupima utendaji kazi ni wa uwazi na umelenga kuhakikisha Mamlaka zinaimarisha ukusanyaji mapato, utoaji huduma na kuzingatia viwango vya

ubora," alisema Mhandisi Fatael.

Mhandisi Fatael alizitaka Mamlaka hizo pia kuhakikisha zinaanda mikataba ya huduma kwa mteja na kusambaza mikataba hiyo kwa wateja wao ili kuhakikisha kuwa wanafahamu haki na wajibu wao katika kupata huduma za maji.

"Upimaji wa utendaji wa mwaka huu (2019) pia utaangalia suala la uwepo wa mkataba wa huduma kwa mteja katika kila mamlaka," alisistiza Mhandisi Fatael.

Kikao kazi hicho kilichofanyika Dar es Salaam hivi karibuni, kilishirikisha zaidi ya wadau 100 kutoka Wizara ya Maji, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na watendaji kutoka Mamlaka za Maji za wilaya, Miji Midogo, Mikoa na Miradi ya Kitaifa.



Washiriki wa kikao kutoka Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Makao Makuu ya Mikoa na Miradi ya Kitaifa, wakiwa kwenye picha ya pamoja hivi karibuni.

# Wadau wafurahishwa ushirikishwaji kwenye uamuzi

By Tobietha Makafu

**W**adau mbalimbali wamefurahishwa na hatua ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kuwashirikisha katika kufanya uamuzi wa masuala ya bei katika masuala yanayogusa maisha yao.

Ushirikishwaji wa wananchi hufanyika kwa njia ya "Taftishi", katika kufanya maamuzi muhimu ikiwemo ya kupanga bei za huduma za maji, umeme na gesi ya kupikia inayoingizwa nchini.

"Taftishi" ni njia ya kufanya uchunguzi wa kina juu ya jambo fulani kabla ya kufanya maamuzi. Kupitia taftishi, EWURA hutafuta maoni ya wadau wa huduma zinazodhibitiwa, ili kufanya maamuzi mbalimbali ikiwemo upangaji wa bei za huduma.

Hivi karibuni EWURA imefanya mikutano ya taftishi za maombi ya kubadili bei za Huduma ya maji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Ngara, Mpwapwa, Shinyanga, Wanging'ombe na Geita. Mamlaka nyingine ni Bunda Karagwe, Turiani, Kigoma, Urambo na Makonde.

Kwa upande wa gesi ya kupikia, taftishi ilifanyika ili kupata maoni ya wananchi juu ya mpango wa kuanza kupanga bei ya gesi hiyo (LPG) ili kuiwezesha EWURA kupanga bei kikomo zitakazotumika kutoa Huduma

hiyo kama inavyofanyika katika kupanga bei za mafuta.

Meneja wa EWURA Nyanda za Juu Kusini Mhandisi Karim Ally, akizungumza kwa niaba ya Mkurugezi Mkuu EWURA, katika taftishi ya Mamlaka ya maji Wang'ing'ombe alisema, "utaratibu wa kukusanya maoni ni moja ya njia za kutekeleza dhana ya Serikali ya utawala bora, kwa maana ya kuwashirikisha wananchi katika kufanya maamuzi muhimu ya kurekebisha bei za huduma za maji kwa kutoa maoni yao kwa uwazi".

Akitoa maoni yake baada ya kuhudhuria taftishi hiyo, mkazi wa Wang'ing'ombe Bi. Fatuma Abdula Mwakifulefule alisema " Tunashukuru EWURA kwa mikutano huu na itakua vizuri kama kweli hizo faida zilizosemwa na mamlaka ya maji, kuboresha huduma, zikifanikiwa na zifanyike kweli."

Baada ya kukusanya maoni ya wadau, EWURA huchambua maoni hayo ili kuhakikisha uamuzi unaotolewa na Mamlaka unakuwa ni wa haki na haupendelei upande wowote.

Kwa mujibu wa Sheria ya EWURA, mtu ye yeyote asiyeridhika na uamuzi wa EWURA kuhusu bei au maamuzi yake yoyote, anayo fursa ya kukata rufaa kwenye Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal (FCT).

**Hivi karibuni  
EWURA imefanya  
mikutano ya taftishi za  
maombi ya kubadili bei za  
Huduma ya maji kwa Mamlaka  
za Majisafi na Usafi wa  
Mazingira za Ngara, Mpwapwa,  
Shinyanga, Wanging'ombe  
na Geita. Mamlaka nyingine  
ni Bunda Karagwe, Turiani,  
Kigoma, Urambo  
na Makonde.**